*Jina la Mwanafunzi*_____ *Namba ya Upimaji*_____

*Shule*_____ *Tarehe*_____

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA

UMOJA WA SHULE ZA MISHENI 0571

ORGANIZATION

UPIMAJI WA PAMOJA AWAMU YA KWANZA, DARASA LA NNE - 2026

L01 SOMO: KISWAHILI

MUDA: Saa 1.30 **Ijumaa, Machi 27, 2026**

Maelekezo:

1. Karatasi hii inasehemu A, B, na C zenye jumla ya maswali matano (5)
2. Jibu maswali yote **kwa usahihi** katika kila sehemu kwa kutumia kalamu ya wino wa **bluu** au **mweusi**
3. Simu za mkononi na vitu vyote visivyoruhusiwa havitakiwi katika chumba cha mtihani/upimaji
4. Andika **jina lako, namba ya upimaji, jina la shule yako, na tarehe ya upimaji** sehemu ya juu katika kila ukurasa

CamScanner

*Jina la Mwanafunzi*_____ *Namba ya Upimaji*_____

*Shule*_____ *Tarehe*_____

Sehemu A (Alama 20): Jibu Maswali yote katika sehemu hii.

1. **Imla: Sikiliza kwa makini sentensi zifuatazo, kisha uziandike kwa usahihi katika nafasi zilizoachwa wazi (Alama 10).**

i. _____
ii. _____
iii. _____
iv. _____
v. _____

2. **Katika kipengele cha (i)-(v), chagua jibu sahihi, kisha andika herufi yake katika mabano yaliyotengwa (Alama 10).**

i. Nusu, robo, na theluthi kwa neno moja ni……
a) uwiano b) vipimo c) vizio d) sehemu [ ]

ii. Umoja wa neno **masega** ni…… [ ]
a) sega b) masega c) segai d) mazega

iii. **'Jino langu linauma'.** Wingi wa neno **jino** ni…….. [ ]
a) majino b) mijino c) mameno d) meno

iv. Mahali ambapo madini huchimbwa hujulikana kama……... [ ]
a) machimbo b) mgodi c) gulio d) mapango

v. **Lango kuu litafungwa saa saba mchana.** Sentensi hii ipo katika wakati gani ?
a) thamani b) samani c) zamani d) dhamani [ ]

vi. **'Mwalimu amekuja'** ukanushi wa sentensi hii ni upi kati ya sentensi zifuatazo ?
a) Mwalimu hajakuja b) Mwalimu hatakuja [ ]
c) Mwalimu hakuja d) Mwalimu hajaja

vii. Ili tufaulu vizuri katika masomo yetu, ……..kusoma kwa bidii.[ ]
a) tana budi b) si budi c) hatuna budi d) ni budi

viii. Tegua kitendawili hiki: 'Kila mtu humwabudu apitapo' [ ]
a) bendera b) kiongozi c) kinyonga d) mlango

ix. Kamilisha sentensi hii: **'Mzee yule hutembelea……'** [ ]
a) bakora b) mkongojo c) mti d) mkoba

x. **Amina ni binti mwerevu.** Kipi ni kinyume cha neno **mwerevu?** [ ]
a) mvivu b) mwaminifu c) mjinga d) muongo

CamScanner

*Jina la Mwanafunzi*_____ *Namba ya Upimaji*_____
*Shule*_____ *Tarehe*_____

3. Methali, Nahau, na Vitendawili (Alama 10)

i. Kamilisha methali hii 'Mwenda tezi na omo .....'

ii. Nini maana ya nahau 'Ingia mitini'? .....

iii. Methali 'Nguzo moja haijengi nyumba' hutufundisha juu ya nini?

.....

iv. Andika kitendawili chenye jibu 'Mbono' .....

v. 'Kila siku ninakufa na kufufuka tena' Jibu ya kitendawili hiki ni nini?

.....

Sehemu B (Alama 10): Jibu maswali yote katika sehemu hii.

4. Utungaji: Soma kwa makini sentensi zifuatazo, kisha zipange kwa kuzipa herufi A, B, C, D, na E katika mtiririko unaoleta maana.

i. Tulimaliza mtihani Ijumaa, saa kumi jioni [ ]

ii. Aliongezea kusema mnatakiwa kujiandaa kwa kujisomea ili kuongeza kumbukumbu [ ]

iii. Mwalimu alitutangazia wanafunzi wa darasa la nne kuwa siku ya Alhamisi na Ijumaa, tutafanya mtihani wa umoja wa shule za misheni [ ]

iv. Mtihani huo utaanza saa mbili na nusu asubuhi, hadi saa kumi jioni, siku zote mbili [ ]

v. Ilipofika Alhamisi, tulianza mtihani [ ]

CamScanner

Jina la Mwanafunzi _____ *Namba ya Upimaji* _____

Shule _____ *Tarehe* _____

Sehemu C (Alama 10): Jibu vipengele vyote katika swali la tano (5)

5. Ufahamu: Soma kwa makini habari ifuatayo, kisha ujibu maswali katika vipengele (i)-(v) vinavyofuata:

Familia ya Mzee Dude ina jumla ya watoto watatu wanaoishi pamoja. Watoto hao ni Zebedayo, Zaituni, na Faraja. Mama wa watoto hao anaitwa Sikudhani. Familia hii inaupendo sana na hushirikiana katika mambo mbalimbali ya familia. Zebedayo ndiye kitinda mimba wa familia hii; yeye hupendwa sana na wanafamilia. Faraja ndiye kifungua mimba katika familia hii. Mzee Dude anawapenda sana watoto wake wote bila ubaguzi.

Maswali

i. Familia ya Mzee Dude ina jumla ya watu wangapi?.....
.....
....

ii. Mtoto wa kwanza katika familia ya mzee Dude anaitwa nani?.....
.....
....

iii. Mzee Dude huwapenda watoto wake wote pasi na.....

iv. Badala ya neno 'familia', mwandishi angeweza kutumia neno lipi lenye maana ya familia?.....
.....

v. Mzee Dude na Mkewe Sikudhani wana jumla ya mabinti wangapi?
.....

CamScanner